ISSN 0856 – 0331X

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TOLEO LA SHERIA

Na. 1 *3 Januari, 2014*

Katika Gazeti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 1 Juzuu ya 95 ya tarehe 3 Januari, 2014

Imepigwa chapa na Mpigachapa Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam kwa amri ya Serikali

SHERIA YA GEPF YA MFUKO WA MAFAO YA WASTAAFU YA MWAKA 2013

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na kuanza kutumika kwa Sheria.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UANZISHWAJI NA USIMAMIZI WA MFUKO

4. Kuanzishwa kwa Mfuko.
5. Mfuko kuwa wakala wa Serikali.
6. Kuanzishwa kwa Mipango ya ziada.
7. Usimamizi wa Mfuko.
8. Kuanzishwa kwa Bodi.
9. Uteuzi wa muundo wa Bodi.
10. Mwenendo wa Bodi.
11. Majukumu ya Bodi.
12. Kazi za Bodi.
13. Kamati za Bodi.
14. Kukasimu mamlaka ya Bodi.
15. Mkurugenzi Mkuu.
16. Uteuzi wa watumishi wa Mfuko.
17. Kuanzishwa kwa Daftari.
18. Taarifa kwa mwanachama.

SEHEMU YA TATU
UANACHAMA KATIKA MFUKO

19. Uanachama wa Mfuko.
20. Ukomo wa uanachama wa mfuko.
21. Umri wa kustaafu.

SEHEMU YA NNE
MICHANGO NA RIBA KWA WANACHAMA

22. Michango ya mwanachama.
23. Ukusanyaji wa michango.
24. Kiwango cha pensheni na kiinua mgongo.
25. Hifadhi ya michango.

SEHEMU YA TANO
FAIDA ZINAZOLIPWA KUTOKA KWENYE MFUKO

26. Haki ya Mafao.
27. Mafao yatakayolipwa chini ya Sheria.
28. Fao la kustaafu.
29. Watu wasiostahili kulipwa pensheni.
30. Fao kwa warithi baada ya kifo.
31. Fao la kutojiweza.
32. Mahesabu ya mafao yatakayolipwa.
33. Marejeo ya hesabu za mafao.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA FEDHA

34. Vyanzo vya mapato.
35. Makadirio ya Bajeti ya mwaka.
36. Mahesabu na Ukaguzi.
37. Msamaha wa Kodi.
38. Taarifa ya mkadiriaji bima.
39. Uwekezaji wa fedha za mfuko.

40. Akaunti za benki za mfuko.
41. Uwezo wa kukopa.
42. Malipo na posho za wajumbe wa Bodi.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI MENGINEYO

43. Kinga dhidi ya kuwajibika kisheria.
44. Mamlaka ya kutunga kanuni.
45. Akaunti ya Akiba.
46. Dhamana ya mkopo wa nyumba.
47. Fursa ya wanachama kutumia sehemu ya mafao yao.
48. Makosa na adhabu.
49. Kufutwa na masharti ya mpito.

JEDWALI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

NA. 8 YA 2013

NAKUBALI,

JAKAYA MRISHO KIKWETE.
Rais

[30 Desemba, 2013]

Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Akiba wa GEPF kwa manufaa ya waajiriwa katika sekta rasmi na isiyo rasmi ikijumuisha watu waliojiari wenyewe, na kwa masuala mengineyo yanayohusiana na hayo.

Imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na kuanza kutumika kwa sheria

1.-(1) Sheria hii inaitwa Sheria ya GEPF ya Mfuko wa Mafao ya Wastaafu ya mwaka 2013.

(2) Sheria hii itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri anaweza kuiteua, kupitia tangazo litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara na itamhusu mtu ambaye-

(a) ameajiriwa katika sekta rasmi au isiyo rasmi; na

(b) amejiajiri mwenyewe,

lakini haijumuishi mtu ambaye amesajiliwa au mwenye bima chini ya sheria nyingine yoyote inayohusiana na hifadhi ya jamii.

Tafsiri

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Masuhuli" maana yake ni mtu mwenye wajibu wa kufanya uhasibu kwa ajili ya huduma yoyote ambayo pesa zimetolewa, na anawajibika kusimamia utendaji na rasilimali za Taasisi;

"Mtakwimu wa Bima" maana yake ni mtu aliebobea katika Sayansi ya mahesabu ya hatari ya Bima na viwango vya malipo na michango;

"Ripoti ya Takwimu ya Bima" maana yake ni ripoti ya tathmini iliyoandaliwa na mtathmini wa Bima chini ya Sheria hii;

"Tathmini ya Takwimu ya Bima" maana yake ni tathmini iliyotengenezwa na Mtakwimu wa Bima;

"Ripoti ya takwimu ya Bima" maana yake ni ripoti ya tathmini iliyoandaliwa na mtathmini wa Bima chini ya sheria hii;

"gharama za kiutawala" maana yake ni gharama zote zitokanazo au zinazohusiana na usajili wa wanachama, ukusanyaji wa michango, ulipaji wa mafao ya wanachama, uwekezaji, michakato ya utoaji maamuzi au utawala;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya jamii iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mdhibiti na Msimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii;

Sura ya 157

"Benki" maana yake ni Benki Kuu ya Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;

"mnu "mnufaika" maana yake ni mtu anayestahili kupokea mafao chini ya Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wadhamini wa Mfuko iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii;

"michango" maana yake ni mchango katika Mfuko unaotolewa kwa masharti ya Sheria hii;

"mwajiri mchangiaji" maana yake ni mwajiri ambaye ana jukumu la kutoa michango kwa ajili ya watumishi wake katika mfuko kwa masharti Sheria hii;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria hii;

"mwajiriwa" maana yake ni mtu ambaye-

(a) ameingia mkataba wa ajira;

(b) ameingia mkataba mwingine wowote ambao anawajibika kufanya kazi kwa upande mwingine wa mkataba na ambapo upande mwingine si mteja wa taaluma, biashara au kazi inayofanywa na mtu huyo;

Sura ya 366

(c) Waziri anamchukulia kuwa ni mwajiriwa chini ya kifungu cha 98(3) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini; au

Sura ya 300

(d) anachukuliwa kuwa ni mwajiriwa kwa mujibu wa kifungu cha 61 cha Sheria ya Taasisi za Ajira:

"mchango wa mwajiriwa" maana yake ni kiwango cha asilimia kilichoainishwa cha mshahara wa mwezi wa mwajiriwa kinacholipwa katika Mfuko;

"mwajiri" ina maana iliyoainishwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini;

"mchango wa mwajiri" maana yake ni kiwango cha asilimia kilichoainishwa cha mshahara wa mwezi wa mwajiriwa ambacho kinalipwa kwenye Mfuko na mwajiri kwa ajili ya mwajiriwa;

"mwaka wa fedha" maana yake ni kipindi cha miezi kumi na mbili kinachoishia tarehe 30 Juni ya kila mwaka;

"sekta rasmi" maana yake ni sekta inayojumuisha mwajiri na waajiriwa ambao wameingia mkataba wa ajira au mafunzo ya kazi au mkataba mwingine wowote uliokusudiwa katika maana ya neno "mwajiriwa";

"mfuko" maana yake ni Mfuko wa Akiba wa GEPF wa Mafao ya Wastaafu ulioanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"muajiriwa wa Serikali" maana yake ni mwajiriwa yeyote katika utumishi wa Serikali;

"sekta isiyo rasmi" maana yake ni sekta inayojumuisha wafanyakazi ambao wanafanya kazi zisizo rasmi na ambao hawafanyi kazi kwa masharti ya mkataba wa ajira au mkataba mwingine wowote uliowekwa katika tafsiri ya neno "mwajiriwa";

"muundo wa lazima" maana yake ni muundo wa lazima ulioanzishwa na sheria na kudhaminiwa na Serikali kutoa mafao ya hifadhi ya jamii kwa waajiriwa;

"Bodi ya utabibu" maana yake ni Bodi iliyoteuliwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya afya kwa madhumuni ya kuamua masuala ya kitabibu chini ya Sheria hii;

"mwanachama wa Mfuko" maana yake ni mwanachama wa Mfuko kufuatana na masharti ya Sheria hii, lakini haijumuishi mwanachama alieteuliwa chini ya kifungu cha 9 na Jedwali katika Sheria hii;

"amana ya mwanachama" maana yake ni michango ya mwajiriwa, michango ya mwajiri na riba yake ambayo ipo kwenye akaunti ya mwanachama;

"Waziri" maana yake ni waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha;

"pensheni ya ujira" maana yake ni mshahara au mapato yatokanayo na mapato ya makato ya michango ambayo itazingatiwa katika ukadiriaji pensheni, au mafao mengine chini ya Sheria hii;

"Daftari" maana yake ni Daftari la wanachama lililoanzishwa chini ya kifungu cha 17;

"Akaunti ya Akiba" maana yake ni akaunti kuu iliyoanzishwa na Bodi chini ya kifungu cha 46;

"mshahara" maana yake ni mshahara wa mwisho mwanachama baada ya makato unaolipwa kwa mwajiriwa kama malipo ya utumishi wake chini ya mkataba wa utumishi au uanagenzi au aina yoyote ya wito isipokuwa bonsai, faida, gharama za maisha, malipo ya muda baada ya kazi, ada ya wakurugenzi au nyongeza nyingine yoyote ya maslahi;

"aliejiajiri" maana yake ni mtu ambaye hafanyi kazi kwa mujibu wa mkataba wa ajira au uanagenzi au mkataba mwingine wowote uliokusudiwa kwenye tafsiri ya neno "mwajiriwa";

"muundo wa hifadhi ya jamii" maana yake ni kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mdhibiti na Msimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii;

"mpango wa hifadhi ya jamii" ina maana iliyotolewa kwake na Sheria ya Mdhibiti na Msimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii;

"muundo wa nyongeza" maana yake ni muundo ulioanzishwa na Bodi kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria hii;

"kiasi kilichotajwa" maana yake ni kiasi kilicho sawa na moja ya tano na themanini na pensheni ya mjumbe kwa kila mwezi uliokusudiwa kipindi cha huduma ambacho kinalipiwa pensheni au vipindi vya uchangiaji;

Sura ya 135

"mpango wa ziada" maana yake ni mpango ulioanzishwa na Bodi kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria hii;

"chama cha wafanyakazi" maana yake ni chama cha wafanyakazi kilichosajiliwa;

"mdhamini" maana yake ni mjumbe wa Bodi ya Wadhamini na inajumuisha Mwenyekiti.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA NA USIMAMIZI WA MFUKO

Kuanzishwa kwa Mfuko

4. Unaanzishwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Mafao ya Wastaafu utakaojulikana kama Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Mafao ya Wastaafu wa GEPF, ambamo ndani yake italipwa-

(a) michango yote itakayohitajika kutolewa chini ya Sheria hii;

(b) fedha zilizopatikana kutokana na mradi wowote, mpango au shughuli ya ujasiriamali inayofadhiliwa na Mfuko;

(c) fedha zilizopatikana kutokana na mali yoyote, uwekezaji, uwekaji rehani, fedha zilizotokana na au kuwekezwa katika Mfuko;

(d) fedha zingine zozote ambazo zimepatikana kihalali zinazotakiwa kulipwa kwa Mfuko; na

(e) Mali zote ambazo zimewekezwa kihalali katika Bodi.

Mfuko kuwa wakala wa Serikali

5.- (1) Mfuko utakuwa ni wakala wa Serikali kwa madhumuni ya malipo ya mafao ya mwisho ya wastaafu.

(2) Mstaafu, chini ya kifungu hiki itajumuisha-

(a) waajiriwa wa Jeshi la polisi na Watumishi wa Magereza ambao hawajachangia kwenye Mfuko kabla ya mwezi wa Julai, mwaka 1999 na ambao kiinua mgongo chao kinapaswa kulipwa na Hazina;

(b) walimu waliaojiriwa chini ya mkataba wa utumishi baada ya kustaafu;

(c) Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya; na

(d) waajiriwa wengine wa Serikali ambao wanaweza kutambulika ipasavyo.

(3) Mfuko utapokea na kutunza michango kutoka Hazina kwa wastaafu waliorejewa katika kifungu kidogo cha (2).

(4) Mfuko utaingia katika mkataba wa uwakala na Serikali ambao utaelezea utaratibu na namna ambavyo majukumu ya wakala na Serikali yatakavyo tekelezwa.

(5) Serikali ita-

(a) lipa kwenye Mfuko ada yoyote ya uwakala na gharama za msingi kwa kiwango ambacho kitakubaliwa kati ya Mfuko na Serikali;

(b) lipa kwenye Mfuko, kwa kila robo mwaka au kwa mwezi, kiasi cha fedha ambacho kitalipwa kama kiinua mgongo kwa wastaafu au warithi wao;

Kuanzishwa kwa mipango ya ziada Sura ya 135.

6.-(1) Bila kujali masharti ya kifungu cha (4), Bodi inaweza kuanzisha mipango ya ziada kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mdhibiti wa Hifadhi ya Jamii.

(2) Bodi inaweza kusimamia mipango ya ziada iliyoanzishwa na mwajiri au mwajiriwa ambaye anadhaminiwa chini ya akaunti tofauti.

Usimamizi wa Mfuko

7.-(1) Bodi itawajibika kwa usimamizi na utawala wa Mfuko kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Sheria ya Mdhibiti wa Hifadhi ya Jamii na kanuni husika.

(2) Bodi itawasilisha kwa Mamlaka taarifa za fedha na taarifa nyingine zozote kuhusiana na shughuli za Mfuko za kila mwaka au katika muda wowote ambao Mamlaka inaweza kuzihitaji.

(3) Taarifa za fedha zilizorejewa katika kifungu kidogo cha (2), zitajumuisha-

(a) hali ya kifedha ya Mfuko;

(b) maelezo ya matumizi ya fedha;

(c) taarifa nyingine yoyote kadri ambavyo Mamlaka inaweza kuhitaji.

Kuanzishwa kwa Bodi

8.-(1) Inaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Wadhamini ya Mfuko.

(2) Bodi itakuwa ni chombo cha kisheria kilicho na uwezo wa kudumu, mhuri rasmi na kwa jina lake la kibiashara, itakuwa na uwezo wa-

(a) kushitaki na kushitakiwa;
(b) kununua au vinginevyo kujipatia, kumilki, kutoza:
(c) kuuza mali yake inayohamishika na mali isiyohamishika;
(d) kukopa na kukopesha;
(e) kuingia katika mikataba; na
(f) kutekeleza majukumu mengine ambayo yanaweza kutekelezwa kihalali na kampuni.

Uteuzi na muundo wa Bodi

9.-(1) Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao-
(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais; na
(b) wajumbe nane watakaoteuliwa na Waziri kama ifuatavyo-
- (i) mwakilishi wa Wizara ya Fedha;
- (ii) Wakili wa Serikali mwenye cheo cha Mfawidhi au zaidi atakayeiwakilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (iii)mwakilishi kutoka katika chama kilicho na uwakilishi wa juu zaidi cha waajiri;
- (iv)wawakilishi wawili wa chama cha waajiri;
- (v) wawakilishi wawili wa chama cha wajumbe waliojiajiri na kutoka katika sekta isiyo rasmi, walio na ujuzi na uzoefu katika mambo ya hifadhi ya jamii;
- (vi)wawakilishi wawili kutoka wajumbe wa Mfuko ambao hawako katika chama chochote cha waajiriwa.

(2) Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni Katibu wa Bodi.

(3)Uchaguzi wa watu kwa uteuzi chini ya kifungu cha 9(1)(b) utazingatia masharti kuhusiana na sifa kama zitakavyo ainishwa na Mamlaka,

Isipokuwa kwamba, masharti yatakayo ainishwa yatazingatia uwakilishi wa kijinsia.

Mwenendo wa Bodi

10.-(1) Masharti yaliyomo kwenye Jedwali yataweka muda wa kuwa madarakani, vikao na taratibu nyingine za Bodi.

(2) Waziri anaweza, kwa Amri itakayo chapishwa katika *Gazeti la Serikali*, kurekebisha, kubadilisha au kuweka masharti mengine badala ya masharti yaliyopo katika Jedwali, isipokuwa kwa aya ya (1) ya jedwali hilo.

Majukumu ya Bodi

11.-(1) Bodi itakuwa na jukumu la ujumla la udhibiti na usimamizi wa Mfuko.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), majukumu ya Bodi yatakuwa ni-

(a) kutunga, kutekeleza na kupitia sera kuhusiana na Mfuko kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(b) kuwekeza fedha za Mfuko kwa uangalifu;

(c) kumshauri Waziri kuhusiana na masuala ya usimamizi wa Sheria;

(d) kutoa mwongozo wakisera na huduma za ushauri kwa madhumuni ya kukuza program za masuala ya hifadhi za jamii; na

(e) kutekeleza mambo yoyote na kuingia. katika mikataba ambayo kwa maoni ya Bodi ni muhimu kwa usimamizi bora wa Mfuko.

Kazi za Bodi

12. Litakuwa ni jukumu la Bodi-

(a) kusimamia Mfuko kwa mujibu wa viwango vya juu zaidi ambavyo mtu aliye na maslahi ya kifedha katika Mfuko mwingine wowote ulioanzishwa na sheria anaweza kutarajiwa kutekeleza;

(b) kulinda na kukuza masuala ya wajumbe wa Bodi; na

(c) katika utekelezaji wa majukumu yake, kutekeleza mkataba wa Bodi na kwa ujumla kukuza misingi ya utawala bora.

Kamati za Bodi

13.-(1) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu yake, Bodi itaanzisha idadi za kamati kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kuhusiana na usimamizi uwekezaji na utawala wa Mfuko.

(2) Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) zitatekeleza majukumu zilizopewa kwa mujibu wa vigezo na masharti kama Bodi itakavyoweza kuamuliwa.

Kukasimu mamlaka ya Bodi

14.-(1) Bodi, kwa maandishi na kwa mhuri wake rasmi na kwa kuzingatia masharti na vigezo ambavyo itaviainisha, inaweza kukasimu yoyote kati ya majukumu yake yaliyoainishwa chini ya Sheria hii, kwa kamati yoyote ya Bodi, Mkurugenzi Mkuu au afisa mwingine yeyote wa Mfuko.

(2) Ukasimishaji unaofanywa chini ya kifungu hiki hautazuia Bodi kutekeleza majukumu iliyoyakasimisha.

(3) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), Bodi haitakuwa na mamlaka ya kukasimu yoyote kati ya majukumu yake yanayohusu uidhinishaji wa bajeti ya mwaka, bajeti ya nyongeza au mahesabu ya mwaka.

Mkurugenzi Mkuu

15.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu atakayeteuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi Mkuu ata-

(a) kuwa ni afisa mtendaji mkuu na Afisa Masuhuli wa Mfuko;

(b) wajibika kwa uangalizi wa shughuli zote za Mfuko;

(c) tunza mhuri wa Mfuko; na

(d) tekeleza majukumu mengine yoyote kwa usimamizi bora wa Mfuko, kwa kadri ambavyo Bodi itaelekeza.

(3) Mkurugenzi Mkuu atakuwa madarakani kwa muda wa miaka mitano na, kwa kuzingatia utekelezaji unaoridhisha, anaweza kuteuliwa tena.

Uteuzi wa watumishi wa Mfuko

16.-(1) Bodi inaweza, kwa masharti na vigezo vya utumishi, kuteua watumishi kwa utekelezaji bora wa majukumu ya Bodi.

(2) Watumishi wa Mfuko watakuwa chini ya uangalizi wa moja kwa moja wa Mkurugenzi Mkuu na wataongozwa na kanuni na taratibu za ndani, kama Bodi itakavyoamua.

Kuanzishwa kwa Daftari

17.-(1) Kunaanzishwa Daftari ambalo ndani yake zitatunzwa kumbukumbu na maelezo ya Mfuko.

(2) Mkurugenzi Mkuu atatunza kumbukumbu na maelezo ya wajumbe wa Mfuko na michango ya Mfuko katika Daftari, katika namna itakayo ainishwa katika Kanuni.

Taarifa kwa wajumbe

18.-(1) Kila mwisho wa mwaka wa fedha, Mkurugenzi Mkuu atatoa kwa kila mwanachama maelezo ya mchango wake.

(2) Mfuko utaitisha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa wajumbe na wadau kwa ajili ya utowaji wa taarifa ya utekelezaji wa Mfuko.

SEHEMU YA TATU
UJUMBE WA MFUKO

Uanachama wa Mfuko

19.-(1) Mtu atawajibika kuwa mwanachama wa Mfuko iwapo mtu huyo ni mwajiriwa katika sekta rasmi au sekta isiyo rasmi na ambaye hajaandikishwa au kudhaminiwa chini ya sheria nyingine yoyote ya hifadhi ya jamii.

(2) Bilakujali masharti ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) raia wa kigeni au raia anaye ishi nje ya nchi anayefanya kazi ndani ya Tanzania katika mradi au muda maalum; au

(b) raia wa Tanzania anayefanya kazi nje ya Tanzania,

anaweza kuchangia katika Mfuko.

Ukomo wa mwanachama wa Mfuko

20.-(1) Mwanachama wa Mfuko atakoma kuwa mwanachama-

(a) atakapo fikia umri uliyotajwa wa kustaafu;

(b) atastaafu kwa sababu za kiafya kutokana na ushahidi utakaoiridhisha Bodi ya Madaktari kuwa mwanachama hana uwezo wa kutekeleza majukumu yake kutokana na sababu ya kutokuwa na akili timamu au udhaifu wa kimwili.

(c) kutokana na ajira ya mwanachama kusitishwa au mwanachama huyo kujiuzulu kutoka katika utumishi wa mwajiri wake na mwanachama huyo anaamua kujiondoa katika uanachama wa Mfuko; au

(d) iwapo mwanachama anafariki.

(2) Mwajiriwa ambaye masharti ya ajira yameisha kabla ya kufikia umri wa kustaafu anaweza kuendelea kuwa mwanachama na kutunza akaunti yake na Mfuko ikiwa ataendelea kuchangia katika Mfuko, katika utaratibu utakaoweza kuamuliwa kati ya Mfuko na mwanachama mwenyewe.

Umri wa kustaafu

21.-(1) Umri wa kustaafu wa hiari utakuwa miaka hamsini na tano.

(2) Mwanachama ambaye anafikia umri wa miaka hamsini na tano anaweza, katika muda wowote baada ya hapo, kuamua kustaafu kwa hiari, isipokuwa kama hajaamua kufanya hivyo, anaweza kuendelea kuwa mjumbe hadi hapo atakapo fikia umri wa miaka sitini.

(3) Wanachama ambao masharti yao ya kisheria ya ajira yanaainisha kipindi kifupi zaidi cha kustaafu kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (2), watastaafu kwa mujibu wa masharti yatakayoainishwa.

SEHEMU YA NNE
MICHANGO NA VIWANGO VYA PENSHENI NA KIINUA MGONGO

Michango ya wajumbe

22.-(1) Mjumbe anayechangia, kwa kila kipindi cha uchangiaji, baada ya siku iliyoteuliwa ambayo mwajiri anamwajiri mjumbe, atalipa kwa Mfuko kiasi cha mchango kitakachokuwa na mchango wa mwajiri na mchango wa mwajiriwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, mchango utachukuliwa, kwa madhumuni ya Sheria hii, kuwa umelipwa kwa Mfuko kwa tarehe ya mwisho ya mwezi huo ambao kuhusiana nao malipo ya mshahara wa mwezi au sehemu ya mshahara wa mwezi yanafanyika kwake, na Afisa Masuhuli atakata mchango huo kutoka katika mshahara wa wajumbe.

(3) kila mchango unaodaiwa chini ya kifungu hiki utalipwa kwa Mfuko ndani ya mwezi mmoja baada ya kuisha kwa mwezi ambao mchango wa mwisho ulilipwa.

(4) Kila mjumbe atachangia kwa Mfuko kiasi kilicho sawa na asilimia moja ya mshahara wake wa mwezi, kwa kila kipindi cha uchangiaji.

(5) Mtu aliyedhaminiwa atachangia katika Mfukio kiasi ambacho ni sawa na asilimia tano ya mshahara wake wa mwezi, ambacho kitakatwa na mwajiri anayechangia kutoka katika mshahara wa mtu huyo anayedhaminiwa, na mwajiri anayechangia atachangia kwa ajili ya mtu huyo aliyedhaminiwa kiasi ambacho ni sawa na asilimia kumi na tano ya mshahara wa mtu huyo aliyedhaminiwa au kiasi ambacho Waziri anaweza, kwa Amri itakayochapishwa katika *Gazeti la Serikali*, kuamua.

(6) Mwajiri au mwajiriwa anaweza kuamua kuchangia kiasi ambacho nikikubwa zaidi ya kile kilichotajwa katika kifungu kidogo cha (5), isipokuwa kwamba kiwango cha mchango wa mwajiriwa hakitazidi asilimia kumi na tano ya michango yote.

(7) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (5), wajumbe waliojiajiri watachangia asilimia mia moja ya michango kama ilivyoainishwa katika Kanuni.

(8) Mfuko utakuwa na haki ya kutoza tozo ya asilimia tano kwa kila mchango uliyocheleweshwa katika namna itakayoainishwa katika Kanuni.

(9) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "kipindi cha uchangiaji" maana yake ni kipindi kinachoishia katika tarehe ya mwisho ya kila mwezi.

Ukusanyaji wa michango

23.-(1) Hatua yoyote ya ukusanyaji wa michango chini ya kifungu cha 48 inaweza kuchukuliwa na Bodi, na iwapo hatua hiyo inachukuliwa mbele ya mahakama, afisa yeyote wa Mfuko au wakili aliyeteuliwa na Mfuko, kwa niaba hiyo, anaweza kufika na kuendesha kesi.

Sura ya 33

(2) Kila mchango halali unaodaiwa kwa Mfuko unaweza kupatikana kwa njia ya kesi chini ya amri ya XXXV ya Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai.

(3) Pale ambapo kosa limetendwa kutokana na sababu ya kutokulipa kwa mchango unaotakiwa kulipwa kwa mujibu wa sheria, hakuna shitaka la jinai litakalofunguliwa pasipo kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kiwango cha pensheni na kiinua mgongo

24.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, mjumbe wa Mfuko ambaye atakuwa na si chini ya takriban miaka kumi na tano ya uchangiaji anaweza, baada ya kustaafu, kustahili ama-

(a) kupata punguzo la pensheni ya mwaka ya kiasi kilichosawa na miezi mitatu hadi minne ya kiasi kilichotajwa;

(b) punguzo la pensheni ya kiinua mgongo iliyosawa na mara kumi na mbili na nusu ya robo ya kiasi kilicho tajwa;

(c) pensheni ya kustaafua ya kila mwezi kwa kiasi cha asilimia thelathini ya kiwango cha mshahara wa mwezi au mapato ya mstaafu yaliyo na nyongeza ya asilimia kumi na tano ya mshahara wake wa kawaida au mapato kwa kila miezi kumi na mbili ya bima ya pensheni ambayo ni nyongeza ya miezi mia moja themanini kwa kiasi cha ukomo wa juu wa asilimia sitini na saba nukta tano (67.5) ya mshahara wa kawaida au mapato; na

(d) malipo ya mkupuo ya pensheni ya miezi ishirini na nne.

(2) Mjumbe ambaye amekuwa anachangia kwa Mfuko kwa miaka kumi na tano au zaidi, atastahili kulipwa pensheni kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) pindi atakapo staafu.

(3) Kwa madhumuni ya kupiga mahesabu ya kiasi cha pensheni au kiinua mgongo ya mjumbe chini ya Sheria hii, kiasi cha kawaida cha ujira cha mjumbe

alichokuwa anapata ndani ya miezi sita kabla ya kustaafu kitatumika katika kupigia mahesabu pensheni au kiinua mgongo chake.

Hifadhi ya michango

25. Kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa mjumbe, kitabaki kuwa mali ya Mfuko, hadi hapo kitakapolipwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, na hakitakuwa sehemu ya mali za mjumbe iwapo anafilisika au mali yake inakamatwa ili kulipia madeni, isipokuwa kama kiasi hicho kinahusiana na mkopo wa nyumba, ambapo mkopaji atakuwa na haki ya kuruhusu kiasi cha mchango wake kutumika kama dhamana kwa mkopo huo.

SEHEMU YA TANO
MAFAO YATOLEWAYO NA MFUKO

Haki ya mafao

26. Endapo mwanachama atakoma kuwa mwanachama kulingana na kifungu cha 20, kiasi kitakachokuwa kimewekwa kwenye mfuko wakati wa kuifunga akaunti hiyo kitalipwa kutoka kwenye Mfuko kwa mwanachama au mtu yeyote ambaye kisheria anastahili.

Mafao yatakayolipwa chini ya Sheria

27.-(1) Mafao yafuatayo yatalipwa chini ya sheria hii-

(a) fao la kustaafu;

(b) fao la warithi;

(c) fao la kutojiweza;

(d) fao la matibabu.

(e) fao la mazishi;

(f) fao la kifo;

(g) fao la elimu.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), Mfuko waweza kubuni mafao mengine.

(3) Waziri kwa amri itakayo chapishwa kwenye Gazeti la Serikali, atatangaza tarehe ambayo mafao yaliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (2) (d) na (f) yatalipwa na kusimamiwa.

Fao la kustaafu

28. Kwa kuzingatia kifungu cha 27 fao la kustaafu litalipwa kwa mtu yeyote ambaye ni mwanachama ambaye amestaafu kutoka kwenye ajira katika umri uliowekwa.

Watu wasiostahili kulipwa pensheni

29. Kila Mwanachama, ambaye ana vigezo vya kulipwa pensheni, ambaye hajatimiza umri wa chini uliowekwa wa miaka kumi na tano wa kuchangia anaweza, wakati wa kustaafu, kupewa kiinua mgongo ambacho hakitazidi mara tano ya kiwango kilichowekwa, ambacho kinachukuliwa kuwa kimehesabiwa kama hakuna kipindi kilichowekwa:

Isipokuwa kwamba malipo chini ya kifungu hiki hayatakuwa chini ya kiwango alichochangia mwanachama na mwajiri, katika mfuko pamoja na riba.

Fao kwa warithi baada ya kifo

30.-(1) Pale mwanachama anapofariki kabla hajatimiza umri uliowekwa wa kustaafu, Bodi itampa wawakilishi wake kiinua mgongo kisichozidi pensheni yake ya mshahara wake wa mwaka au mahesabu yake ya kiinua mgongo, kama yapo ambalo ni kubwa.

(2) Mkurugenzi Mkuu anaweza, baada ya kujiridhisha kwa ushahidi uliotolewa, atalipa kwa mrithi kulingana na utaratibu uliowekwa katika Kanuni na vifungu vya sheria vinavyohusiana na usimamizi wa mali za marehemu.

Fao la kutojiweza

31.-(1) Fao la kutojiweza litakalo tolewa chini ya kifungu hiki litalipwa kwa mwanachama ambaye kimwili au kiakili ni mlemavu kiasi cha kumfanya mtu huyo asiweze kuajiriwa.

(2) Vigezo na utaratibu uliowekwa wa usimamizi wa mafao chini ya kifungu hiki utakuwa kama utakavyowekwa katika Kanuni.

Mahesabu ya mafao yatakayolipwa

32. Mkurugenzi Mkuu atafanya mahesabu ya malipo ya mafao ya mwanachama, na taratibu za kulipa mafao zitakuwa kama itakavyoainishwa kwenye kanuni.

Marejeo ya hesabu za mafao

33.-(1) Mwanachama yeyote ambaye hajaridhika wa mafao chini ya kifungu cha 32 anaweza, ndani ya miezi sita baada ya maamuzi ya Mkurugenzi Mkuu, kuiomba Bodi kwa maandishi ifanye marejeo.

(2) Bodi itapitia na kutoa maamuzi chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa namna iliyowekwa katika Kanuni.

Sura ya 135

(3) Mwanachama asiyeridhishwa na maamuzi ya Bodi anaweza kukata rufaa kwa Mamlaka kwa namna iliyowekwa chini ya Sheria ya Mamlaka Udhibiti wa Mifuko ya Ustawi wa Jamii.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya mapato

34. Vyanzo vya mapato vitajumuisha -
(a) michango ya wanachama;
(b) michango ya waajiri;
(c) fedha zinazotokana na uwekezaji;
(d) kiasi cha fedha ambacho kitapitishwa na Bunge kwa ajili ya Mfuko;
(e) kiasi chochote cha fedha ambacho kimekopwa na Bodi kulingana na masharti ya Sheria hii;
(f) fedha zinazopatikana kutokana na zawadi au msaada; na
(g) chanzo kingine chochote halali cha fedha kilichopo katika Mfuko.

Makadirio ya Bajeti ya mwaka

35.-(1) Kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha Mkurugenzi Mkuu, ataandaa au atawezesha kuandaliwa kwa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha unaofuatia na kuyawasilisha kwenye Bodi.

(2) Baada ya kupokea makadirio kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), Bodi itayaangalia na kuyachukua makadirio hayo kulingana na marekebisho kama Bodi itakavyoona inafaa.

(3) Makadirio ya Bajeti ya mwaka yataweka masharti kwa makadirio yote ya matumizi kwa mwaka ujao wa fedha na yatahusu-
(a) malipo ya mafao kwa wanachama;

(b) malipo ya mishahara, posho na gharama nyingine zinazohusu Bodi, Kamati za Bodi na watumishi wa Mfuko;

(c) malipo kwa ajili ya ujenzi, matengenezo ya majengo au mali za Mfuko zisizohamishika;

(d) malipo kwa ajili ya matengenezo na ununuzi wa samani na vifaa vingine vya Mfuko; na

(e) kuanzisha mfuko wa akiba kwa ajili ya kutimiza majukumu ya matumizi kadri Bodi itakavyoona inafaa.

(4) Matumizi hayatafanywa kwa ajili ya Mfuko isipokuwa kulingana na masharti ya makadirio ya bajeti ya mwaka au makadirio ya Nyongeza yatakayofanywa na Bodi.

(5) Usimamizi wa mwaka wa matumizi ya mfuko hayatazidi asilimia kumi na tano ya mapato yote ya mfuko.

(6) Nakala ya Makadirio ya mwaka baada ya kuidhinishwa na Bodi itapelekwa kwa Waziri.

(7) Bajeti itakayoidhinishwa na Bodi itatumika kulingana na matumizi yaliyoainishwa ya Mfuko na kwa kiasi kilichoainishwa kwenye bajeti ya mwaka au bajeti ya nyongeza.

(8) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (6)-

(a) Bodi inaweza-

(i) kuhamisha kiasi kutoka kwenye matumizi yaliyowekwa kwa ajili ya Bajeti kuu kulingana na kitu chochote,ambacho kimewekwa katika bajeti iliyopita na kinyume chake; au

(ii) kubadilisha kiwango cha matumizi kulingana na mazingira ambayo hayakuonekana wakati wa kuandaa bajeti, kulingana na kuwasilisha kwa bajeti ya nyongeza katika Bodi ndani ya miezi miwili ya mabadiliko hayo ya matumizi; na

THIS BOOK BELONGS TO THE LIBRARY OF THE ATTORNEY GENERAL'S CHAMBERS

(b) Mkurugenzi Mkuu anaweza kubadili matumizi ya fedha kutoka kifungu kimoja cha bajeti kwenda kifungu kingine ndani ya usimamizi uliowekwa au matumizi.

Mahesabu na Ukaguzi

36.-(1) Hesabu za Mfuko yatafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au kampuni nyingine ya ukaguzi iliyoidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(2) Hesabu za Mfuko, ndani ya miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha kumalizika, zitawasilishwa kwa ukaguzi.

(3) Hesabu zote zilizokaguliwa zitawasilishwa kwenye mkutano wa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa na kupokelewa.

(4) Bodi, Mara baada ya hesabu za Mfuko kukaguliwa, na kwa namna yoyote si zaidi ya miezi sita baada ya mwaka wa fedha kumalizika, itawasilisha nakala ya taarifa za hesabu zilizokaguliwa pamoja na nakala ya taarifa kwa Waziri, Mamlaka na Benki.

(5) Waziri baada ya kupokea taarifa iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (4) atawasilisha Bungeni taarifa itakayokuwa na-

(a) nakala ya taarifa za hesabu za Mfuko zilizokaguliwa; na

(b) nakala ya taarifa kuhusu shughuli za Mfuko kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Msamaha wa kodi

37.-(1) Kodi ya Ushuru wa stempu, na Kodi ya ushuru wa bidhaa na ongezeko la thamani haitatozwa kwenye risiti, hati ya mkataba au nyaraka zozote inazotolewa na Bodi kwa niaba ya Mfuko au mtu yeyote anayepokea mafao au marejesho ya michango chini ya Sheria hii.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), kifungu hiki hakitatafsiriwa kutoa msamaha kwa mtu ambaye anawajibika kulipia ushuru wa stempu au aliyepewa mamlaka kisheria kulipwa kwa niaba yake au nyaraka yoyote ambayo ingetakiwa kulipiwa kodi hiyo chini ya Sheria ya Kodi ya ushuru wa stamp.

Sura ya 189

(3) Kodi ya Mapato juu ya michango na mafao yaliyolipwa chini ya mpango au kodi ya makampuni au kodi yoyote ambayo inaweza kuwasilishwa kwenye mfuko haitatakiwa kuwasilishwa katika Mfuko.

Taarifa ya mkadiriaji bima

38.-(1) Kila baada ya miaka mitatu au ndani ya muda ambao Bodi inaweza kuelekeza, Mamlaka itawezesha mali na madeni ya Mfuko kuthaminishwa na Mkadiriaji bima.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Bodi inaweza kulipa kulingana na asili na mazingira ya utendaji wa mfuko, kwa ruhusa ya Mamlaka, chini ya kifungu kidogo cha (1).

(3) Taarifa ya uthamini itawasilishwa kwenye Mamlaka na kwa Waziri.

(4) Baada ya kupokea taarifa, mamlaka inaweza kuelekeza Mfuko kuchukua hatua zinazostahili kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa katika taarifa.

Uwekezaji wa fedha za mfuko

39.-(1) Bodi inaweza kuwekeza fedha za Mfuko katika vitega uchumi ambayo itaona vinafaa, na uwekezaji utafanyika baada ya Bodi kujiridhisha kuwa vitega uchumi hivyo vinalipa.

(2) Kwa kuzingatia usahihi wa biashara inayokusudiwa kufanyiwa uwekezaji, Bodi itazingatia uhalisia wa kiuchumi na kibiashara wa biashara hiyo na miongozo kama itakavyotolewa chini ya Sheria ya Mdhibiti na Msimamizi wa Hifadhi ya Jamii.

Sura ya 135

(3) Iwapo uwekezaji utafanywa kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1), kila mwanachama wa Bodi ya wadhamini, mkurugenzi, meneja au afisa yeyote wa Mfuko aliyeshiriki katika kufanya maamuzi ya uwekezaji atawajibika yeye mwenyewe kulipa faini kama ilivyoelekezwa chini ya Sheria ya Mdhibiti na Msimamizi wa Hifadhi ya Jamii.

(4) Bila kujali adhabu iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3) Benki Kuu itakuwa na mamlaka ya-

(a) kusimamia Mfuko ili uweze kuzingatia taratibu za uwekezaji;

(b) kusitisha uwekezaji; au

(c) kuchukua hatua nyingine yoyote inayoona kuwa inafaa.

Akaunti za benki za Mfuko

40. Mfuko utamiliki akaunti moja ya benki au zaidi kama Bodi itakavyoidhinisha, kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na Mamlaka ambamo fedha zote zinazolipwa kwenye Mfuko na mapato yote yanayotokana na uwekezaji wa Mfuko zitawekwa.

Uwezo wa kukopa

41. Bodi inaweza, baada ya kupata idhini ya Waziri, kukopa fedha kwa madhumuni ya shughuli za Bodi kwa njia ya mkopo au mkopo wa deni katika akaunti ya Benki, kwa dhamana na masharti yanayohusiana na ulipaji wa kiasi kilichokopwa pamoja na riba, kama Bodi inavyoona inafaa.

Marupurupu na posho za wajumbe wa Bodi

42. Wajumbe wa Bodi watastahili kulipwa malipo ambayo yameidhinishwa na Waziri, baada ya kupokea mapendekezo ya Bodi.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI MENGINEYO

Kinga dhidi ya kuwajibika kisheria

43. Tendo au jambo lolote lililofanywa, au ambalo halijafanywa na mdhamini yeyote, au mwajiriwa au wakala wa Mfuko halitamfanya mtu huyo achukuliwe hatua au awajibishwe iwapo jambo hilo limefanywa au halijafanywa kwa nia njema katika kutekeleza au dhana ya utekelezaji wa majukumu yake kama mdhamini, mwajiriwa wa Mfuko au wakala.

Mamlaka ya kutunga Kanuni

44.-(1) Waziri baada ya kushauriana na Bodi, anaweza kutunga Kanuni kwa lengo la kutekeleza masharti ya Sheria hii kikamilifu.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), waziri anaweza kutunga Kanuni zinaelezea-

(a) utaratibu wa kuchangia kwenye mfuko;
(b) utaratibu wa kusimamia mafao yanayotolewa chini ya sheria hii;
(c) namna ya kutumia fedha zilizopo kwenye akaunti ya Mfuko na ambazo hakuna madai halali yaliyofanywa ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu kiasi hicho cha fedha kilipopaswa kulipwa kulingana na masharti ya Sheria hii;
(d) utaratibu wa namna mfuko utakavyoweka na kutunza taarifa za wanachama; na
(e) suala jingine muhimu kwa madhumuni ya usimamizi bora wa Mfuko ikiwa ni pamoja na kufafanua wajibu wa wadau, waajiri na wanufaishwa.

Akaunti ya Akiba

45.-(1) Bodi itaanzisha, kutunza, na kusimamia Akaunti ya Akiba ambayo ndani yake-
(a) zitawekwa fedha zitakazolipwa kwenye Akaunti ya Akiba kwa mujibu wa Sheria hii; na
(b) zitawekwa faini zitakazotozwa chini ya Sheria hii.

(2) Fedha zitakazolipwa kwenye Akaunti ya Akiba kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), zinaweza kutumika zote au sehemu yake kufidia hasara na kulipa gharama nyingine kama itakavyoamuliwa na Bodi.

Dhamana ya mkopo wa nyumba

46. Mwanachama wa Mfuko anaweza kutumia sehemu ya mafao yake kama dhamana ya mkopo wa nyumba ya makazi kulingana na utaratibu ulioelekezwa na Mamlaka.

Adhabu kwa ucheleweshaji wa ulipaji wa mafao

47.-(1) Mwajiri, ndani ya kipindi cha miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu kwa mwajiriwa, ataufahamisha Mfuko kwa maandishi kuhusu tarehe ya kustaafu kwa mwajiriwa husika.

(2) Mfuko utahakikisha kwamba, baada ya kupokea taarifa ya kustaafu kwa mwajiriwa ambaye ni mwanachama, unamlipa mwanachama huyo mafao yake ya kustaafu anayostahili ndani ya siku sitini.

(3) Pale ambapo Mfuko utashindwa kumlipa mwanachama mafao ya kustaafu ndani ya kipindi kilichoainishwa katika kifungu kidogo cha (2), na mwanachama hakusababisha kushindwa huko, Mfuko utamlipa mwanachama huyo kiasi cha jumla ya mafao anayostahili kama malipo ya kustaafu, pamoja na asilimia kumi na tano ya kiasi hicho kwa mwaka kama adhabu.

Makosa na adhabu

48.-(1) Mtu yeyote ambaye -

(a) kwa makusudi atatoa kutoka kwenye mshahara wa mtumishi ambaye anachangia kwenye mfuko, kiasi cha fedha ambazo ni zaidi ya kiwango kilichowekwa kisheria;

(b) kwa lengo la kujipatia faida au malipo kwa ajili yake au mtu mwingine yeyote, kwa makusudi anatoa taarifa za uongo au anamwakilisha mtu mwingine, anawasilisha au anasababisha kuwasilishwa kwa taarifa ambazo anajua ni za uongo;

(c) bila kuwa na sababu ya msingi, atashindwa kuwasilisha kwenye mfuko, fomu za mwanachama ambaye mafao yake yameiva;

(d) atadanganya au kushindwa kutoa taarifa sahihi;

(e) akiwa ni mwajiri atashindwa kuwasilisha michango ya watumishi wake wanaochangia kwenye mfuko, na kusababishia watumishi hao kutokuingiziwa michango yao;

(f) atakiuka masharti ya sheria hii pale ambapo hakuna adhabu iliyoainishwa,

atakuwa ametenda kosa na atawajibika, baada ya kutiwa hatiani-

(i) ikiwa kosa limetendeka chini ya kifungu cha (1)(a),(b),(c) na (e) kulipa faini isiyopungua mara mbili ya kiasi cha hasara iliyotokea au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote;

(ii) ikiwa kosa limetendeka chini ya kifungu kidogo (1) (d) na (f) atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni mbili au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote.

(2) Pamoja na adhabu zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1)(i), mahakama itatoa amri ya ulipwaji wa gharama ya hasara iliyopatikana.

Kufutwa na masharti ya mpito
Sura ya 51

49.-(1) Sheria ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali ya mwaka 1942 inafutwa.

(2) Bila kujali kufutwa kwa Sheria ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali-

(a) waajiri na wanachama wote waliokuwa wanachangia mfuko chini ya Sheria iliyofutwa watatambulika kuwa wamechangia chini ya Sheria hii;

(b) maelekezo yote yaliyotolewa chini ya Sheria iliyofutwa na ambayo yanaendelea kutekelezwa mara kabla ya kuanza kwa Sheria hii yataendelea kutumika hadi hapo yatakapotolewa chini ya Sheria hii.

(c) Sheria Ndogo zote zilizotengenezwa chini ya Sheria iliyofutwa zitatambulika kuwa zimetengenezwa chini ya Sheria hii na zitaendelea kutumika hadi hapo zitakapofutwa au kutenguliwa na Sheria Ndogo zitakazotengenezwa chini ya Sheria hii;

(d) mamlaka, haki, marupurupu, majukumu na stahili au madeni ambayo kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii yalikuwepo kwa mujibu wa sheria iliyofutwa yatatambulika kuwa yamewekwa chini ya Sheria hii;

(e) teuzi zote na hatua zilizochukuliwa kihalali chini ya Sheria iliyofutwa zitaendelea kuwa halali hadi zitakapofutwa au kubadilishwa chini ya Sheria hii au kanuni;

(f) mali zote na madeni yaliyokuwepo mara kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii yatakabidhiwa kwenye mfuko pamoja na haki na wajibu unaotokana na mkataba wowote au vinginevyo utaendelea kama vile Sheria hii haijaanza kutumika;

(g) kila kitu kilichofanyika au hatua iliyochukuliwa chini ya sheria iliyofutwa kama haitakinzana na masharti ya Sheria hii, itatambulika kuwa imefanyika au imeelekezwa chini ya masharti yanayowiana katika Sheria hii;

(h) ikiwa mara kabla ya kuanza kwa Sheria hii-

(i) mtu aliwajibika kulipa kiasi cha fedha kwenye Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini kutokana na deni ambalo alikuwa akidaiwa chini ya sheria inayofutwa, . mtu huyo anapaswa kufanya malipo hayo kwenye Mfuko kama vile deni hilo linatokana na Sheria hii; na

(ii) shauri lolote linalotokana na kosa lililotendeka chini ya sheria inayofutwa au kwa ajili ya kukusanya kiasi cha fedha zilizokuwa zinadaiwa chini ya sheria iliyofutwa, ambalo linaendelea katika mahakama yoyote, litaendelea kama vile limefunguliwa chini ya Sheria hii.

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 10)

MASHARTI YANAYOHUSIANA NA BODI

Muda wa uteuzi

1.-(1) Kila mjumbe wa Bodi ataendelea kushika nafasi hiyo kwa miaka mitatu kuanzia tarehe aliyoteuliwa na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine.

(2) Bila kuathiri aya ya (1), mjumbe anaweza kujiuzulu muda wowote kwa kutoa notisi ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi na atakoma kuwa mjumbe kuanzia tarehe iliyotajwa kwenye notisi na endapo hakuna tarehe iliyotajwa kwenye notisi, kuanzia tarehe ambayo mamlaka ya uteuzi itaipokea notisi hiyo.

(3) Mtu ambaye ni mjumbe kutokana na kuwa mtumishi katika ofisi nyingine, atakoma kuwa mjumbe pindi atakapoacha kuwa mtumishi kwenye ofisi ambayo kwayo alikuwa mjumbe.

Kusitishwa kwa uteuzi

2. Pale mjumbe yeyote wa Bodi ataacha kuhudhuria vikao vitatu vya Bodi mfululizo bila sababu ya msingi, Bodi itaishauri mamlaka ya uteuzi kuhusu kutokahudhuria huko na mamlaka ya uteuzi itaweza kusitisha uteuzi wa mjumbe huyo na kumteua mjumbe mwingine kushika nafasi yake.

Kukoma kwa mjumbe

3. Pale mjumbe wa Bodi atakapokoma kuwa mjumbe kwa sababu ya kujiuzulu au kifo au akishindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya kuwa nje ya nchi au kwa sababu ya ulemavu au ugonjwa wa akili au endapo mamlaka ya uteuzi itasitisha uteuzi wake chini ya aya ya 2, mamlaka ya uteuzi itaweza kumteua mjumbe mwingine kushika nafasi yake, na mjumbe atakayeteuliwa atashika nafasi hiyo kwa mujibu wa jedwali hili kwa kipindi kilichobaki cha mtangulizi wake kwa muda uliobakia wa mjumbe aliyetangulia.

Makamu Mwenyekiti

4. Bodi itamteua mmoja wa wajumbe wake kuwa Makamu Mwenyekiti na endapo ataendelea kuwa mjumbe, atashika wadhifa huo wa Makamu Mwenyekiti kwa kipindi kitakachowekwa na Bodi na ataweza kuteuliwa kwa kipindi kingine baada ya muda huo kwisha.

Mamlaka ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti

5. -(1) Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya Bodi.

(2) Endapo kwenye kikao chochote cha Bodi Mwenyekiti hatakuwepo, Makamu Mwenyekiti atakiongoza kikao hicho.

(3) Endapo wote Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawatakuwepo kwenye kikao chochote cha Bodi, wajumbe watakaokuwepo watamteua mmoja kati yako kuwa Mwenyekiti wa muda ambaye atakiongoza kikao hicho.

(4) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mwenyekiti wa muda watakuwa na haki ya kupiga kura, na endapo kura zitafungana, watakuwa na kura ya ziada ya turufu.

Mikutano na utaratibu wa kuendesha mikutano

6.-(1) Mkutano wa kawaida wa Bodi utaitishwa na Mwenyekiti na notisi/taarifa inayoainisha mahali, tarehe na muda wa mkutano itatumwa kwa kila mjumbe kupitia sehemu yake ya kawaida anapofanyia shughuli au anapoishi katika kipindi kisichopungua siku kumi na nne kabla ya tarehe ya mkutano huo.

(2) Bodi itafanya mikutano yake ya kawaida mara nne kwa mwaka, isipokuwa Mwenyekiti anaweza kuitisha mkutano wa dharura pale patakapokuwa na haja ya kufanya hiyo.

(3) Mwenyekiti wa Bodi anaweza kumkaribisha mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Bodi kushiriki katika majadiliano ya vikao vya Bodi lakini mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Akidi

7.-(1) Akidi ya kikao chochote cha Bodi itakuwa ni nusu ya wajumbe wote.

(2) Endapo Mwenyekiti hatakuwepo kwenye kikao cha Bodi, wajumbe waliopo watamteua mjumbe mmoja kati yako kuwa Mwenyekiti wa muda wa kikao hicho.

Maamuzi kwa kusambaza nyaraka

8.-(1) Bila kujali masharti ya aya ya 3, pale mwenyekiti atakapoelekeza, maamuzi yanaweza kufanywa na Bodi bila kufanya mkutano kwa kusambaza nyaraka muhimu kwa wajumbe wote na watatoa maoni yako kwa maandishi.

(2) Mjumbe yeyote anaweza kupendekeza maamuzi hayo yasizingatiwe na suala hilo lishughulikiwe kwenye kikao cha Bodi.

Dondoo za kikao

9. Dondoo za kila kikao cha Bodi zilizowekwa katika mfumo sahihi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na zitasainiwa na Mwenyekiti kwenye kikao.

Uhalali wa lakiri

10. Lakiri ya Bodi haitawekwa kwenye hati au nyaraka yoyote isipokuwa kwa kushuhudiwa na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu au kwa kushuhudiwa na aidha Mwenyekiti ama Mkurugenzi Mkuu na mjumbe mmoja wa Bodi atakayeteuliwa na Bodi kwa ajili hiyo.

Kutiwa saini kwa nyaraka

11. Nyaraka zote ambazo Bodi inahusika isipokuwa nyaraka ambazo zinapaswa kisheria kuwekwa lakiri, maamuzi yote ya Bodi yanaweza kutiwa saini na Mkurugenzi Mkuu au afisa mwingine atakayeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu kwa ajili hiyo.

Uhalali wa vikao

12. Hakuna jambo au kikao cha Bodi kitakachokuwa batili kwa sababu ya kutotimia kwa akidi wakati jambo au kikao hicho kikifanyika au mapungufu katika uteuzi wa mjumbe yeyote au kutokana na ukweli kwamba mjumbe yeyote alibatilishwa au hakustahili kushiriki wakati wa jambo au kikao hicho.

Bodi kujiwekea utaratibu

13. Kwa kuzingatia masharti ya jedwali hili, Bodi yaweza kujiwekea utaratibu.

Umepitishwa na Bunge tarehe 5 Novemba, 2013.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH,
Katibu wa Bunge